

# HALMASHAURI YA WILAYA YA MBEYA

Tel:025 - 2502260  
 Fax: 025 - 2500128  
 MKURUGENZI MTENDAJI:  
 Baruapepe:[mbeyaded@yahoo.com](mailto:mbeyaded@yahoo.com)  
 Kumb. Na. MDC



S.L.P.599,  
 MBEYA.  
 TANZANIA

13/03/2017

## TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI KWA KIPINDI CHA JULAI - FEBRUARY, 2017

Ifuatayo ni taarifa ya mapato na matumizi kwa kipindi cha Julai – Februari, 2017.

### 1.1 MAPATO

Kwa mwaka wafedha 2016/2017, Halmashauri imekadiria kukusanya na kupokea jumla ya Sh. **41,735,051,800**. Kati ya fedha hizo Sh. **3,549,678,000** ni kutoka vyanzo vya ndani (Own Source) na Sh. **38,185,373,800** ni Ruzu kutoka Serikali Kuu na Wahisani.

Katika kipindi cha Julai–February,2017, Halmashauri imeweza kukusanya na kupokea jumla ya Sh. **28,340,973,765** sawa na asilimia **65** ya makadirio, ambapo mapato toka vyanzo vya ndani ni Sh. **1,313,124,952** sawa na asilimia **37** ya makadirio na Ruzuku toka Serikali Kuu na Wahisani ni Sh. **27,027,848,813** na asilimia **49** ya makadirio.

Aidha Halmashauri inayo bajeti timilizi ya Sh. **1,969,099,100**.

Jedwali la mapato ya ndani na Ruzuku kwa Julai–Februari ni kama inavyoonesha hapa chini

MAELEZO	BAJETI			HALISI			
	Makisio 2016/2017	BajetiTimilizi	Jumla	Makusanyo 2016/2017	BajetiTimilizi	Jumla	%
Mapatoya Ndani	3,549,678,000	2,986,234	3,552,664,234	1,310,138,718	2,986,234	1,313,124,952	37
Ruzuku OC	2,224,038,000	18,268	2,224,056,268	895,452,760	18,268	895,471,028	45
Ruzuku PE	30,596,206,000	91,009,641	30,687,215,641	20,834,024,800	91,009,641	20,925,034,441	62
Ruzuku Miradi	5,365,129,800	1,875,084,958	7,240,214,758	3,332,258,387	1,875,084,957	5,207,343,344	63
<b>JUMLA</b>	<b>41,735,051,800</b>	<b>1,969,099,101</b>	<b>43,704,150,901</b>	<b>26,371,874,665</b>	<b>1,969,099,100</b>	<b>27,027,848,813</b>	<b>57</b>

Aidha kwa mwezi February, 2017, Halmashauri imeweza kukusanya na kupokea jumla ya Sh.**2,707,693,436** sawa na asilimia **81** ya makadirio kwa mwezi, ambapo mapato toka vyanzo vya ndani ni Sh.**140,444,211** sawa na asilimia **48** ya makadirio ya mwezi, Ruzuku toka Serikali Kuu (OC) ni Sh.**6,949,000** sawa na asilimia **4**, Ruzuku (PE) ni Sh. **2,562,249,225** sawa na asilimia **100** na Ruzuku ya Miradi ya Maendeleo ni Sh. **0** sawa na asilimia **0** ya makadirio kwa mwezi.

Jedwali la Mapato ya Ndani na Ruzuku kwa mwezi Februari, 2017 ,ni kama inavyoonekana hapa chini.

Maelezo	Makisio Februari 2017	Mapato Halisi Februari, 2017	%
---------	-----------------------	------------------------------	---

Mapato ya Ndani	295,806,500	140,444,211	48
Ruzuku OC	185,336,500	6,949,000	75
Ruzuku PE	2,549,683,833	2,562,249,225	100
Ruzuku Miradi	327,607,250	-	0
<b>Jumla</b>	<b>3,358,434,083</b>	<b>2,709,642,436</b>	<b>81</b>

Muhtasari wa mapato umeonyeshwa katika ukurasa wa 5 na mchanganuo wake umeonyeshwa katika ukurasa wa 6 – 9 wa taarifa hii.

Mh. Mwenyekiti, katika kipindi hiki cha Julai – Februari, 2017 kuna vianzia vikuu vilivyo fanya vizuri kwa kufikia **58%** au zaidi ya makadirio. Vianzia hivyo ni kama ifuatavyo;

#### **Leseni za Biashara 60%**

**Sababu;**Ukaguzi unafanyika na kikosi kazi kinacho ongozwa na Afisa Biashara (W) ilikubaini wafanya biashara ambao leseni zao zimeisha muda wake. Hatua za kisheria zinachukuliwa kwa wafanya biashara wanao kiuka sheria za leseni.

#### **Leseni zaVileo 78%**

**Sababu;**Ukaguzi unafanyika na kikosi kazi kinachoongozwa na Afisa Biashara (W) ilikubaini wafanya biashara ambao leseni zao zimeisha muda wake. Hatua za kisheria zina chukuliwa kwa wafanya biashara wanaokiuka sheria za leseni.

#### **Ada ya Mabango 83%**

**Sababu;** Ilani zilitolewa,ufuatiliaji umefanyika kwa makampuni na wafanya biashara wa kawaida.

#### **Mazao ya Misitu ya Serikali 60%**

**Sababu;** Kianza hiki kina kusanywa na Halmashauri kupitia Wakala wa Misitu ya Kiwirana Kawetire, uvunaji unaendelea kwasasa.

Mh. Mwenyekiti, katika kipindi hiki, pia kuna vianzia ambavyo havijafanya vizuri kwa kutofikia **58%**. Vianzia hivyo na sababu zake ni kama ifuatavyo;

#### **Ukodishaji wa mali za Halmashauri 46%**

Kianza hiki ukusanyaji unaendelea, matangazo yametolewa kwa wale ambao hawapo tayari kulipaTsh 50,000 hawatapewa mkataba.

#### **Ushuru wa Mazao ya Chakula 8%**

**Sababu;**Kianza hiki kimeathirika sana na ukosefu wa mvua hasa kwa zao la viazi msimu wa kwanza tumeshindwa kukusanya kwa kiwango tulichotarajia.

#### **Ushuruwa Kahawa 48%**

**Sababu;** Kianza hiki kinakusanywa na Halmashauri kupitia Bodi ya Kahawa (TCB) ambapo ,makusanyo ya naendelea.

#### **Ada ya Uzoaji Taka 1%**

**Sababu;** **Sababu;** Kianza hiki kinakusanywa na Halmashauri yenyewe. Changamoto iliyopo ni upatikanaji wa usafiri wa uhakika kwaajili ya kuzoa taka. Gari linalotumika pamoja na trekta ni machakavu yamekuwa yakiharibika mara kwa mara.

## **1.2 FEDHA ZA RUZUKU ZILIZOPOKELEWA FBRUARI, 2017.**

	<b>Maelezo</b>	<b>Kiasi</b>
1.	Posho ya madaraka/ Elimu bila malipo	-
2.	Mradi wa maji	-
3.	Mfuko wa Barabara (Road Fund)	-
4.	P4R	-
	<b>Jumla</b>	-

## 2. MATUMIZI

Kwa mwaka wa fedha **2016/2017**, Halmashauri imekadiria kutumia jumla ya Sh. **41,735,051,800**. ikiwani kwaajili ya kugharamia shughuli za uendeshaji, mishahara ya watumishi na miradi ya maendeleo.

Katika kipindi cha Julai - February, 2017, Halmashauri imetumia TSh.**23,371,642,190** sawa na asilimia **60** ya makadirio, ambapo matumizi kwaajili ya Mishaharani TSh.**18,984,366,105**

sawa na asilimia **62** ya makadirio, matumizi mengineyoni TSh. **1,398,817,091** sawa na asilimia **23** na matumizi ya Miradi ya Maendeleo ni TSh. **2,988,458,994** sawa na asilimia **44**.

Haliya matumizi ni kama inavyoonesha katika jedwali hapa chini.

<b>MAELEZO</b>	<b>BAJETI</b>			Matumizi Halisi Julai -Februari, 2017	%
	Makisio 2016/2017	Bajeti Timilizi	Jumla		
Matumizi Mengineyo	5,773,716,000	3,004,502	5,776,720,502	1,398,817,091	25
Ruzuku ya Mishahara	30,596,206,000	91,009,641	30,687,215,641	18,984,366,105	62
Ruzuku ya Miradi ya Maendeleo	5,365,093,800	1,875,084,958	5,806,371,958	2,988,458,994	56
<b>Jumla</b>	<b>41,735,015,800</b>	<b>1,969,099,100</b>	<b>42,091,594,441</b>	<b>23,371,642,190</b>	<b>56</b>

Katika kipindi cha mwezi February, 2017, Halmashauri imetumia Sh. **3,124,345,800** sawa na asilimia **94** ya makadirio, ambapo matumizi kwaajili ya mishahara ya watumishi ni Sh. **2,562,249,225** sawa na asilimia **100** ya makadirio, matumizi mengineyo ni Sh. **226,968,380** sawa na asilimia **44** na miradi ya maendeleo ni Sh. **332,128,195** sawa na asilimia **114** ya makadirio.

Hali ya matumizi ni kama inavyoonesha jedwali hapa chini.

<b>Maelezo</b>	<b>Makisio Februari, 2017</b>	<b>Matumizi Halisi Februari, 2017</b>	<b>Asilimia (%)</b>
Matumizi Mengineyo	481,143,000	226,968,380	48
Ruzukuya Mishahara	2,549,683,833	2,565,249,225	100
Ruzukuya Miradi	327,607,250	332,128,195	100.02
<b>Jumla</b>	<b>3,358,434,083</b>	<b>3,124,345,800</b>	<b>93</b>

Mchanganuo wa matumizi umeoneshwa katika ukurasa wa 1-36 wataarifa ya Epicor.

## 3. Bakaa ya Fedha

	<b>Jina la Akaunti</b>	<b>Salio Disemba 31, 2016</b>	<b>Salio Februari, 31, 2017</b>
1	Afya	563,006,524.25	712,939,834
2	Amana	149,984,542	226,287,922
3	Elimu	16,031,920	45,630,000
4	Mishahara	27,890,769.52	0
5	OC	34,819,685	18,201,360
6	Maji	855,340,984.95	858,135,658
7	Maendeleo	810,000,104.71	727,157,246
8	MapatoyaNdani	162,214,997.55	115,008,864
9	Barabara	734,346,927.97	587,065,499
	<b>Jumla</b>	<b>3,290,209,649.36</b>	<b>3,290,426,383</b>